JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
WIZARA YA KILIMO

TOZO, ADA NA KODI 105 ZILIZOFUTWA NA SERIKALI YA AWAMU YA TANO KATIKA BODI NA TAASISI ZILIZO CHINI YA WIZARA YA KILIMO MWAKA 2015 - 2020

DESEMBA, 2020

1.0 UTANGULIZI

Serikali ya Awamu ya Tano imedhamiria kuweka mazingira wezeshi ya biashara na uwekezaji kwa lengo la kuongeza tija na uzalishaji wa mazao ya kilimo kwa kufanya maboresho ya Sera na sheria mbalimbali. Tozo na Ada katika uzalishaji wa mazao zinaweza kuwa na athari hasi kwa wakulima, kutokana na baadhi ya tozo hizo kutozwa moja kwa moja kwa wakulima, na hivyo kupunguza mapato yao. Aidha, baadhi ya Kodi na Tozo zinazotozwa kwa wafanyabiashara zimekuwa zikiathiri ushindani wa biashara ya mazao ya Kilimo kwa kuongeza gharama za biashara na hivyo wafanyabiashara kurudisha gharama hizo kwa wakulima kwa kupunguza bei ya mazao kwa wakulima.

Katika kipindi cha miaka mitano (2015-2020), Serikali imefanya maboresho ya Kodi, Ada na Tozo mbalimbali katika sekta mbalimbali za uchumi ikiwemo sekta ya kilimo (mazao). Maboresho hayo ni utekelezaji wa Programu ya Kuendeleza Sekta ya Kilimo Awamu ya Pili (ASDP II) hususan eneo Kuu la Nne linalohusu Kuiwezesha Sekta katika Uratibu, Ufuatiliaji na Tathmini na utekelezaji wa Mpango

wa kuboresha Mfumo wa udhibiti wa Biashara (Blueprint for Regulatory Reforms to Improve the Business Environment).

Katika kipindi cha miaka mitano (5) Serikali imefanya maboresho ya ada na tozo kwa kufuta jumla ya tozo na ada 105 zilizokuwa zinatozwa kupitia bodi na taasisi zilizo chini ya Wizara ya kilimo kama inavyoonesha katika jedwali hapa chini:

NA.	ZAO/TAASISI	IDADI YA ADA/TOZO ZILIZOFUTWA
1	TUMBAKU	10
2	KAHAWA	20
3	KOROSHO	6
4	MIWA/SUKARI	17
5	PAMBA	4
6	CHAI	5
7	MBEGU	12
8	MBOLEA	4
9	USHIRIKA	26
10	MFUKO WA PEMBEJEO	1
11	**JUMLA**	**105**

Ufafanuzi wa aina ya tozo, kodi na ada zilizofutwa na Serikali kwa mazao ya kimkakati katika bodi na Taasisi ni kama ifuatavyo:

2.0 ZAO LA TUMBAKU

i. Tozo ya Dhamana ya Benki Kuu ya Tanzania kwa ajili ya mikopo (1% Loan guarantee);

ii. Tozo ya shilingi 200,000 kwa ajili ya fomu ya Maombi ya Leseni za kununua Tumbaku (License Application Form fee);

iii. Tozo ya shilingi 8,000,000 kwa ajili ya leseni ya Kununua Tumbaku Kavu aina ya moshi (Dark Fire Cured Tobacco- DFC licence fee);

iv. Tozo ya shilingi 8,000,000 kwa ajili ya leseni ya Kununua Tumbaku mbichi Kiwandani aina ya mvuke (Virginia Flue Cured Tobacco-VFC),(Green Leaf Tobacco Buying License fee at Factory - VFC);

v. Tozo ya shilingi 8,000,000 kwa ajili ya leseni ya Kununua Tumbaku mbichi Kiwandani aina ya moshi (Dark Fire Cured Tobacco-DFC), (Green Leaf Tobacco Buying License fee at Factory-DFC);

vi. Tozo ya kiasi cha USD 3,500 kwa ajili ya leseni ya Kununua Tumbaku mbichi aina ya Mvuke (Virginia Flue Cured Tobacco-VFC) kwa kila Wilaya. (Green Leaf Tobacco Buying License fee per District;

vii. Tozo ya kiasi cha USD 3,500 kwa ajili ya leseni ya Kununua Tumbaku mbichi aina ya moshi (Dark Fire Cured Tobacco- DFC) kwa kila Wilaya, (Green Leaf Tobacco Buying License fee per District;

viii. Tozo ya kiasi cha USD 4,000 kwa ajili ya leseni ya Kuuza Tumbaku nje ya nchi (Tobacco export licence fee);

ix. Tozo ya kiasi cha USD 0.01 kwa Kilo kwa ajili ya mchango wa Baraza la Tumbaku (Tobacco Council Fee -0.01 Per Kg);

x. Tozo ya asilimia 0.25 ya gharama za kuagiza (Green leaf tobacco import licence fee of 0.25% of import value) kwa ajili ya leseni ya kuagiza Tumbaku mbichi nje ya nchi.

3.0 ZAO LA KAHAWA

i. Ada ya leseni ya kuuza nje ya nchi Kahawa ya kijani (Green Coffee Export License) kwa Kampuni na Vyama vya Ushirika (Tsh 2,000,000);

ii. Ada ya leseni ya ghala la kahawa (Warehouse license) kwa Kampuni na Vyama vya Ushirika (Tsh 1,000,000);

iii. Ada ya leseni ya curing/hulling license kwa Kampuni na Vyama vya Ushirika (Tsh 2,000,000);

iv. Ada ya leseni ya premium coffee exports kwa Kampuni (Tsh 2,000,000);

v. Ada ya leseni ya premium coffee exports kwa Vyama vya Ushirika (Tsh1,000,000);

vi. Ada ya leseni ya kuuza nje ya nchi kahawa iliyosindikwa (Roast beans and Instant Coffee Export) kwa Kampuni na Vyama vya Ushirika (Tsh1,000,000);

vii. Ada ya leseni ya kununua kahawa (Parchment/dry cherry coffee buying license) kwa Kampuni tu (Hakuna Ada kwa Vyama vya Ushirika) (Tsh 2,000,000);

viii. Tozo ya Fomu ya kuomba leseni ya kuuza nje Kahawa ya kijani (Green Coffee Export License) kwa Kampuni na Vyama vya Ushirika (Tsh40,000);

ix. Tozo ya Fomu ya kuomba leseni ya ghala la kahawa (Warehouse license) kwa Kampuni na Vyama vya Ushirika (Tsh 40,000);

x. Tozo ya Fomu ya kuomba leseni ya curing/ hulling license kwa Kampuni na Vyama vya Ushirika (Tsh 40,000);

xi. Tozo ya Fomu ya kuomba leseni ya premium coffee exports kwa Kampuni (Tsh 40,000);

xii. Tozo ya Fomu ya kuomba leseni ya premium coffee exports kwa Vyama vya Ushirika (Tsh40,000);

xiii. Tozo ya Fomu ya kuomba leseni ya kuuza nje ya nchi kahawa iliyosindikwa (Roast beans

and Instant Coffee Export) kwa Kampuni na Vyama vya Ushirika (Tsh 40,000);

xiv. Tozo ya Fomu ya kuomba leseni kwa usindikaji wa ndani (Local roasting license) kwa Kampuni na Vyama vya Ushirika (Tsh 40,000);

xv. Ada ya fomu ya leseni ya usindikaji kahawa (Cherry Processing License) (USD 20);

xvi. Tozo ya Fomu ya kuomba leseni ya kununua kahawa (Parchment/dry cherry coffee buying license) kwa Kampuni tu (Hakuna Ada kwa Vyama vya Ushirika) (Tsh 40,000);

xvii. Tozo ya uendeshaji wa minada ya Bodi ya Kahawa ambapo wanunuzi huchangia 0.2 ya mauzo ya kahawa wanayonunua mnadani;

xviii. Ada ya Ukaguzi wa viwango kwa zao la Kahawa zinazochangwa kupitia viwanda vya kusindika kahawa;

xix. Mchango kwa ajili ya mfuko wa kahawa (Tanzania Coffee Development Trust Fund)

unaochangiwa na wazalishaji na wanunuzi kwa kiwango cha 0.1 ya mauzo ya kahawa;

xx. Ushuru wa Kahawa inayouzwa nje ya nchi kupitia mnada kwa kiwango cha asilimia 0.25 ya bei ya mnadani ***(Export fee of auction price of coffee).***

4.0 ZAO LA KOROSHO

i. Tozo ya gharama za magunia na kamba (Tsh. 56 kwa Kilo);

ii. Tozo ya leseni ya ununuzi wa korosho kwa kiwango cha (Tsh 2,000,000);

iii. Ada ya Ukaguzi wa viwango kwa zao Korosho zinazochagwa kupitia viwanda vya korosho;

iv. Tozo ya Chama Kikuu cha Ushirika wa Shilingi 20 kwa Kilo;

v. Tozo ya Kikosi Kazi kwa ajili ya ufuatiliaji wa shughuli za masoko ya korosho Shilingi 10;

vi. Tozo ya Unyaufu wa korosho iliyohifadhiwa kwenye maghala shilingi 10 kwa Kilo.

5.0 ZAO LA SUKARI/MIWA

i. Ada ya leseni ya uingizaji wa Sukari ya viwandani kiasi cha Shilingi 200,000;

ii. Ada ya leseni ya uingizaji wa Sukari ya kuziba pengo (gap-sugar) kiasi cha Shilingi 200,000;

iii. Ada ya leseni Kamili ya uzalishaji sukari uwekezaji mkubwa mpya USD 30,000 (Licensing Sugar Millers - New Establishment- Full license);

iv. Ada ya leseni ya Muda ya uzalishaji sukari uwekezaji mkubwa mpya USD 20,000 (Licensing Sugar Millers - New Establishment- Provisional license);

v. Ada ya leseni Kamili ya uzalishaji sukari uwekezaji mdogo mpya USD 5,000 (Licensing Sugar Min - New Establishment- Full license);

vi. Ada ya leseni ya muda ya uzalishaji sukari uwekezaji mdogo mpya USD 2,500 (Licensing Sugar Min - New Establishment, Provisional - Min license);

vii. Leseni ya marudio kila baada ya miaka mitatu uwekezaji mkubwa TZS 20,000,000 (Licensing Sugar Millers - Renewals for existing after three years large Millers);

viii. Tozo ya Leseni Kamili, marudio kila baada ya miaka mitatu uwekezaji mdogo TZS 5,000,000 (Licensing Sugar Millers - Renewals for existing after three years mini Millers Full license);

ix. Leseni ya Muda marudio kila baada ya miaka mitatu uwekezaji mdogo TZS 2,000,000 (Licensing Sugar Millers - Renewals for existing after three years mini Millers Full license);

x. Leseni ya kuchakata sukari guru TZS 250,000 (Licensing Jaggery Millers);

xi. Ada ya kusajili waagizaji wakubwa wa sukari ya viwandani (above 5000MT) TZS 5,000,000;

xii. Ada ya kusajili waagizaji wa kati wa sukari ya viwandani (1001 - 5000MT) TZS 2,000,000;

xiii. Ada ya kusajili waagizaji wadogo wa sukari ya viwandani (above 5000MT) TZS 500,000;

xiv. Ada ya kusajili wafanyabiashara wa sukari ya matumizi ya kawaida TZS 2,000,000;

xv. Ada ya kupata kibali cha kuingiza sukari ya viwandani kila mwaka TZS 200,000;

xvi. Ada ya kupata kibali cha kuingiza sukari ya kuziba pengo kila mwaka TZS 1,000,000.

xvii. Ada ya leseni ya kuuza nje ya nchi molasses TZS 500,000.

6.0 ZAO LA PAMBA

i. Tozo ya Kituo cha kununulia pamba katika ngazi ya Halmashauri (Tsh. 5,000) (NB: Mnunuzi mmoja anaweza kuwa na vituo hadi 500);

ii. Tozo ya maendeleo ya elimu inayotozwa kwa kiwango cha shilingi 10 kwa kilo katika Halmashauri ya Meatu;

iii. Mchango kwa ajili ya maendeleo ya zao la

pamba fedha ambazo huwekwa kwenye mfuko wa maendeleo ya zao la pamba kwa ajili ya kusaidia kutoa mbegu na dawa za pamba (Tsh. 30 kwa Kilo);

iv. Tozo ya mchango wa Mwenge kwa kila kiwanda cha kuchambua pamba wa Shilingi 450,000.

7.0 ZAO LA CHAI

i. Tozo ya gharama za uendeshaji wa Vyama vya Wakulima (Tsh 5 kwa kilo);

ii. Ada ya Ukaguzi wa viwango kwa zao la chai huchajiwa kupitia viwanda vya kusindika chai;

iii. Ushuru wa Chai (Tea Import Cess) ambayo hutozwa kiasi cha USD 0.0125 kwa Kilo, kwa Kampuni ambazo huingiza chai kutoka nje ya nchi kwa ajili ya kuchanganya na chai ya ndani;

iv. Mchango kwa ajili ya utafiti wa zao la chai Tsh. 9.50/= kwa Kilo ya chai kavu;

v. Tozo kwa ajili ya mkutano wa wadau kiwango cha Tsh. 2 kwa kilo.

8.0 TAASISI YA UDHIBITI WA UBORA WA MBEGU TANZANIA

i. Tozo ya Fomu ya usajili wa muuza mbegu (dealers) kwa kiwango cha Tsh. 2,500;

ii. Tozo ya Fomu ya majaribio ya DUS kwa kiwango cha Tsh. 2,500;

iii. Tozo ya Fomu ya Majaribio ya NPT kwa kiwango cha Tsh. 2,500;

iv. Tozo ya Fomu ya ukaguzi wa mbegu mashambani kwa kiwango cha Tsh. 3,500;

v. Tozo ya Fomu ya majaribio ya mbegu kwa kila lot kwa kiwango cha Tsh. 2,000;

vi. Tozo ya Kibali cha kusafirisha mbegu kwa kiwango cha Tsh. 2,500;

vii. Tozo ya Fomu ya Tangazo (Notice) ya kusafirisha au kuagiza mbegu Tsh. 2,500;

viii. Ada kwa ajili ya Cheti cha usajili na utambuzi (Certificate and tags) kwa muuza mbegu

kwa kiwango cha 100,000 na USD 50;

ix. Ada kwa ajili ya Cheti cha usajili wa aina za mbegu (Variety registration certificate) kwa kiwango cha 50,000 na USD 25;

x. Ada kwa ajili ya Cheti cha majaribio ya mbegu (certificate of seed testing) kwa kiwango cha 5,000 na USD 2;

xi. Ada kwa ajili ya cheti cha majaribio ya DUS (DUS test certificate) kwa kiwango cha Tsh. 5,000 au USD 2;

xii. Ada ya kuthibitisha nakala ya cheti (certified copy of a certificate) kwa kiwango cha Tsh. 2,500 au USD 1.

9.0 MAMLAKA YA UDHIBITI WA MBOLEA TANZANIA

i. Tozo kwa ajili wa usajili wa Mfanyabiashara (Dealer) wa mbolea kiwango cha Tsh. 100,000;

ii. Ada ya leseni ya Mfanyabiashara (Dealer) wa mbolea kiwango cha Tsh. 40,000;

iii. Ada ya Usajili wa Mbolea (Registration of Products) kiwango cha Tsh. 100,000;

iv. Ada ya Usajili wa Mzalishaji wa mbolea *(Sterilizing plants or Manufacturer)* kiwango cha 2,000,000.

10.0 TUME YA MAENDELEO YA USHIRIKA

i. Ada ya usajili wa marekebisho ya Masharti ya Chama cha Ushirika cha Msingi kwa kiwango cha Tsh. 20,000;

ii. Ada ya usajili wa marekebisho ya Masharti ya Chama cha Ushirika cha Upili kwa kiwango cha Tsh. 40,000;

iii. Ada ya usajili wa marekebisho ya Masharti ya Chama cha Ushirika cha Kati kwa kiwango cha Tsh. 80,000;

iv. Ada ya usajili wa marekebisho ya Masharti ya Chama cha Ushirika Shirikisho kwa kiwango cha Tsh. 200,000;

v. Ada ya usajili wa marekebisho ya Masharti ya Chama cha Ushirika katika uwekezaji wa pamoja kwa kiwango cha Tsh. 80,000;

vi. Ada ya uchunguzi kwenye Rejista ya Chama cha Ushirika cha Msingi kwa kiwango cha Tsh. 5,000;

vii. Ada ya uchunguzi kwenye Rejista ya Chama cha Ushirika cha Upili kwa kiwango cha Tsh. 10,000;

viii. Ada ya uchunguzi kwenye Rejista ya Chama cha Ushirika cha Kati kwa kiwango cha Tsh. 20,000;

ix. Ada ya uchunguzi kwenye Rejista ya Shirikisho la Vyama vya Ushirika kwa kiwango cha Tsh. 20,000;

x. Ada ya uchunguzi kwenye Rejista ya Chama cha Ushirika kwa ajili ya uwekezaji wa pamoja kwa kiwango cha Tsh. 15,000;

xi. Ada ya ukaguzi wa kumbukumbu au taarifa za Chama cha Ushirika cha Msingi kwa kiwango cha Tsh. 5,000;

xii. Ada ya ukaguzi wa kumbukumbu au taarifa za Chama cha Ushirika cha Upili kwa kiwango cha Tsh. 10,000;

xiii. Ada ya ukaguzi wa kumbukumbu au taarifa za Chama cha Ushirika cha Kati kwa kiwango cha Tsh. 15,000;

xiv. Ada ya ukaguzi wa kumbukumbu au taarifa za Shirikisho la Vyama vya Ushirika kwa kiwango cha Tsh. 20,000;

xv. Ada ya ukaguzi wa kumbukumbu au taarifa za Chama cha Ushirika kwa ajili ya uwekezaji wa pamoja kwa kiwango cha Tsh. 15,000;

xvi. Ada ya utoaji wa nakala za nyaraka zilizothibitishwa au ambazo hazijathibitishwa kwa Chama cha Ushirika cha Msingi kwa kiwango cha Tsh. 10,000;

xvii. Ada ya utoaji wa nakala za nyaraka zilizothibitishwa au ambazo hazijathibitishwa kwa Chama cha Ushirika cha Upili kwa kiwango cha Tsh. 20,000;

xviii. Ada ya utoaji wa nakala za nyaraka zilizothibitishwa au ambazo hazijathibitishwa kwa Chama cha Ushirika cha Kati kwa kiwango cha Tsh. 30,000;

xix. Ada ya utoaji wa nakala za nyaraka zilizothibitishwa au ambazo hazijathibitishwa kwa Shirikisho la Vyama vya Ushirika kwa kiwango cha Tsh. 60,000;

xx. Ada ya utoaji wa nakala za nyaraka zilizothibitishwa au ambazo hazijathibitishwa kwa Chama cha Ushirika kwa ajili ya uwekezaji wa pamoja kwa kiwango cha Tsh. 20,000;

xxi. Ada ya utoaji wa barua ya kutambua chama cha ushirika cha awali kwa kiwango cha Tsh. 20,000;

xxii. Ada ya utoaji wa Cheti cha Usajili na Masharti kwa Chama cha Ushirika cha Msingi kwa kiwango cha Tsh. 50,000;

xxiii. Ada ya utoaji wa Cheti cha Usajili na Masharti kwa Chama cha Ushirika cha Upili kwa kiwango cha Tsh. 100,000;

xxiv. Ada ya utoaji wa Cheti cha Usajili na Masharti kwa Chama kingine cha Ushirika cha Kati kwa kiwango cha Tsh 200,000;

xxv. Ada ya utoaji wa Cheti cha Usajili na Masharti kwa Shirikisho kwa kiwango cha Tsh. 1,000,000;

xxvi. Ada ya utoaji wa Cheti cha Usajili na Masharti kwa uwekezaji wa pamoja kwa kiwango cha Tsh. 100,000.

11.0 MFUKO WA TAIFA WA PEMBEJEO

i. Ada ya Nyaraka (documentation fee) ambayo ni asilimia 1 ya thamani ya mkopo.

12.0 TOZO NA ADA ZILIZOPUNGUZWA VIWANGO

i. Tozo ya leseni ya Kununua Tumbaku Kavu (VFC) (Dry Leaf Tobacco Buying License (Domestic sales) - VFC). Tozo hiyo imepungua kiwango kwa asilimia 50 kutoka Shilingi 8,000,000 hadi shilingi 4,000,000;

ii. Leseni ya Kusindika Tumbaku (Tobacco Processing License) Tozo hiyo imepungua kiwango kwa asilimia 50 kutoka shilingi 20,000,000 shilingi 10,000,000;

iii. Tozo kwa ajili ya kugharamia shughuli za utafiti wa zao la kahawa. Tozo hiyo imepunguzwa kiwango kwa asilimia 50 kutoka asilimia 0.75 ya bei ya kahawa hadi asilimia 0.375 ya bei ya kahawa ya mnadani;

iv. Tozo ya uhakiki wa ubora wa mbolea kabla ya kuanza kutumika nchini. Tozo hiyo imepunguzwa kiwango kutoka Dola za Kimarekani 30,000 hadi Dola za Kimarekani 10,000 kwa msimu mmoja.

KWA MAWASILIANO

KATIBU MKUU
WIZARA YA KILIMO,
MJI WA SERIKALI, MTUMBA,
S.L.P. 2182,
DODOMA.
Simu: 255(026) 2321407
Nukushi: 255 (026)2320037
Barua pepe: ps@kilimo.go.tz,
Tovuti: www.kilimo.go.tz